## IJUE OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

### 1.0 UTANGULIZI

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ni taasisi kuu ya ukaguzi katika sekta ya umma kwenye Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na imekuwepo tangu zama za ukoloni ikiendesha shughuli zake kwa kuzingatia Sheria, kanuni na miongozo mbalimbali kulingana na wakati husika.

Wakati wa utawala wa Mwingereza Ofisi ilijulikana kama Idara ya Ukaguzi ya Kikoloni na ilikuwa ikiripoti kwa Gavana ambaye alimwakilisha Malkia wa Uingereza. Wakati huo maafisa waligawanywa katika madaraja makuu matatu ambayo ni Ajira ya Mafao ya Ulaya, ngazi ya maafisa (Europian Pension Scheme-Officers Rank), Ajira ya Mafao ya Asia, ngazi ya ukaguzi wa hesabu (Asian Pension Scheme - Examiners of Accounts) na Ajira ya Mafao ya Afrika, ngazi ya makarani wa ukaguzi (Audit Clerks).

Kipindi chote hiki, Ofisi hii ilikuwa ikiongozwa na Mkurugenzi wa Ukaguzi (Director of Audit) kwa mujibu wa Sheria ya Ukaguzi Sura 386 (Audit Ordinance Cap. 386) hadi ilipoanzishwa Sheria ya Fedha na Ukaguzi ya mwaka 1961 (Exchequer and Audit Ordinance 1961) iliyobadilisha jina la cheo cha mkuu wa taasisi hii kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Wakati na baada ya Uhuru, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imekuwa ikijitegemea kimuundo na kiutendaji kama ilivyo ainishwa katika Katiba ya Tanganyika ya mwaka 1961, ibara ya 73 ambayo ilitambua uwepo na kutoa mamlaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambaye ndio kiongozi Mkuu wa Taasisi kama inavyoonekana pia katika Katiba ya mwaka 1977.

Hivi sasa mamlaka na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali umefafanuliwa na kuanishwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa mwaka mara kwa mara) pamoja na Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Na. 11 ya mwaka 2008.



*Prof. Mussa Juma Assad, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) - 2014 hadi Sasa*



*Bw. Ludovick S. L. Utouh, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali(CAG) – 2006 hadi 2014*



*Bw. Thomas Kiama, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) – 1996 hadi 2005*



*Bw. Mohamed Aboud, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) – 1969 hadi 1996*



*Mr. Gordon A. Hutchinson, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali(CAG) – 1964 hadi 1969*

## 2.0 DIRA, DHIMA NA MAADILI YA MSINGI

### 2.1 Dira

Dira ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali inalenga katika kuwa kituo bora cha ukaguzi wa hesabu katika sekta ya umma.

### 2.2 Dhima

Dhima ya Ofisi hii ni kutoa huduma bora za ukaguzi wa hesabu zenye kuleta tija kwa nia ya kuimarisha uwajibikaji na thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma.

### 2.3 Maadili ya Msingi

- ✓ Kutopendelea - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi isiyopendelea, inayotoa huduma kwa wateja wake kwa haki.

- ✓ Ubora - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni ya kitaalamu inayotoa huduma bora za ukaguzi wa hesabu kwa kuzingatia viwango vya kitaaluma.

- ✓ Uadilifu - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inazingatia na kudumisha haki kwa kiwango cha juu na kuheshimu sheria.

- ✓ Zingatio kwa Wadau - Tunalenga matakwa ya wadau wetu kwa kujenga utamanduni wa kutoa huduma bora kwa wateja na kuwa na watumishi wenye uwezo na ari ya kazi.

- ✓ Ubunifu - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi bunifu ambayo wakati wote inaimarisha na kukaribisha mawazo mapya ya kimaendeleo toka ndani na nje ya taasisi.



## 3.0 MAJUKUMU YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Kama ilivyofafanuliwa katika ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anajukumu la kufanya ukaguzi wa hesabu za fedha na kutoa ripoti angalau mara moja kwa mwaka, pia kuhakikisha kwamba fedha zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na matumizi yake yanafanywa kwa kuzingatia masharti ya ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo iwapo atatosheka kwamba masharti hayo yametekelezwa ipasavyo, basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe na hilo ndiyo jukumu la udhibiti kwa mujibu wa katiba ya nchi yetu.

Katiba hiyo hiyo inasisitiza kuwa katika kutekeleza majukumu yake, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu hatalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu mwingine yeyote au idara yoyote ya Serikali. Hata hivyo Mahakama imepewa nguvu katika ibara ndogo ya 143 ya kuchunguza kama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ametekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kadri itavyoona inafaa.

## 4.0 MFUMO WA UWAJIBIKAJI UNAOFUATWA NA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inafuata mfumo wa uwajibikaji wa ‘Westminster’ kutoka Uingereza. Mfumo huu unaonesha mahusiano kati ya Bunge, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na Watendaji wa serikali/ Maafisa Masuuli kama ifuatavyo:



Bunge linampa wajibu Afisa Masuuli kusimamia fedha na utoaji wa huduma, taratibu za uwajibikaji kuweka pamoja taarifa za upimaji. Wajibu wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika mchakato huu ni kukagua taarifa ya fedha iliyowasilishwa na watendaji wa serikali na kutoa ripoti yake kwa Bunge. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu anaweza pia kutoa taarifa juu ya uzingatiaji wa ubanifu, tija na ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za serikali. Ripoti ya ukaguzi ni hatua ya kwanza katika ngazi ya uangalizi. Anayewakilisha Bunge, Kamati ya Usimamizi ni wadau wakuu wa ripoti ya ukaguzi.

## 5.0 HATUA ZA UTOAJI WA TAARIFA ZA UKAGUZI NA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YATOLEWAYO RIPOTI ZA UKAGUZI




## 6.0 JE CAG ANAKAGULIWA NA NANI

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kama zilivyo Taasisi nyingine za Umma hukaguliwa kila mwaka na ripoti yake ya ukaguzi kuwasilishwa Bungeni. Kwa mujibu waSheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008 Kifungu 46 (1) hadi (6) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma inatoa utaratibu wa kumpata Mkaguzi wa kuikagua Ofisi ya Taifa ya ukaguzi wa Hesabu za Serikali. Sheria hiyo inaeleza kuwa Mkaguzi anayekagua hesabu za Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali atachaguliwa na Kamati ya Hesabu za Serikali Kuu (yaani PAC) kutoka kwenye makampuni binafsi ya ukaguzi (Private Audit Firms) yanayotambuliwa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA).

## 7.0 MAFANIKIO YA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Katika kuisaidia Serikali kuboresha taarifa zake za mapato na matumizi, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inajivunia mafanikio mbalimbali katika ngazi ya kitaifa na kimataifa.

- ✓ Mafanikio ya ngazi ya kitaifa ni pamoja na uboreshwaji wa taarifa za fedha na hati za ukaguzi. Idadi ya taasisi za serikali zilizokuwa zinapata Hati zenye Shaka zilikuwa zinakaribiana na zile zilizokuwa zinapata Hati zinazoridhisha. Kwa sasa hali ni tofauti sana kwani hati zinazoridhisha zimeongezeka na hati zisizoridhisha zimepungua mno ukilinganisha na miaka ya nyuma. Kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2015 CAG alitoa jumla ya Hati za Ukaguzi 465 zinazohusu Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma. Kadhalika, alitoa Hati 799 zinazohusu Miradi ya Maendeleo kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali hapa chini.

| Na. | Taasisi zilizokaguliwa | Idadi ya Taasisi zilizokaguliwa | Aina ya hati za ukaguzi | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Hati Safi | Hati yenye shaka | Hati isiyoridhisha | Hati mbaya |
| 1 | Halmashauri (S/Mitaa) | 164 | 47 | 113 | 3 | 1 |
| 2 | Serikali Kuu | 199 | 180 | 18 | 1 | 0 |
| 3 | Mashirika ya Umma | 102 | 99 | 3 | 0 | 0 |
| | **Jumla Ndogo** | **465** | **326** | **134** | **4** | **1** |
| | **Asilimia** | **100%** | **70%** | **28.8%** | **1%** | **0.2%** |
| 4 | Miradi | 799 | 739 | 60 | 0 | 0 |
| | **Jumla Kuu** | **1,264** | **1065** | **194** | **4**[1] | **1**[2] |

- ✓ Aidha, suala la kutolewa kwa Hati za ukaguzi zinazoridhisha na Hati zenye Shaka lilikuwa mojawapo ya meseji kuu zilizotolewa katika Ripoti za kila mwaka za CAG kuhusu kaguzi mbalimbali alizokuwa anazifanya katika Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma. Lazima tukiri kwamba kwenye kipindi cha miaka michache iliyopita, mojawapo ya matukio ambayo sasa yanasubiriwa kwa hamu hapa nchini ni lile la kuwasilishwa kwa ripoti za CAG kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hatimaye kuwasilishwa na kujadiliwa Bungeni. Ofisi itajielekeza zaidi katika kuboresha mahusiano na wadau wake kwa lengo la kuimarisha misingi ya uwajibikaji ambapo msisitizo mkubwa utawekwa kwa taasisi zitakazopata hati zenye shaka.

[1] Shirika la Mzinga, Halmashauri za Wilaya ya; Hai, Kigoma Ujiji na Karatu
[2] Halmashauri ya Mji wa Tunduma

- ✓ Kwa upande wa Ukaguzi wa Ufanisi, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amefanikiwa kufanya kaguzi na jumla ya kutoa ripoti 45 hadi kufikia tarehe 31 Machi 2016. Ufafanuzi wa idadi za ripoti Ukaguzi wa Ufanisi kwa kila mwaka ni kama ifuatavyo:

| S/N | Mwaka | Idadi ya Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi |
|---|---|---|
| 1. | 2007 | 1 |
| 2. | 2010 | 6 |
| 3. | 2011 | 2 |
| 4. | 2012 | 6 |
| 5. | 2013 | 5 |
| 6. | 2014 | 7 |
| 7. | 2015 | 6 |
| 8. | 2016 | 12 |
| **Jumla** | | **45** |

- ✓ Kaguzi hizi za ufanisi pia zimegusa maeneo mbalimbali ya kijamii ikiwa ni pamoja na Elimu, Afya, Maji, Mazingira, Kilimo, Shughuli za Mafuta na Gesi, Miundo Mbinu, Mifugo, Maliasili. Lengo za kaguzi hizo ni kutoa mapendekezo ya kuboresha shughuli zilizoangaliwa kutokana na tatizo lililoonekana.

- ✓ Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu siyo tu ni ripoti ambazo kwa sasa serikali inazisubiri kwa hamu bali ni ripoti ambazo vyombo vya habari na Watanzania kwa ujumla wao wanazifuatilia kwa karibu. Ni wazi kwamba hali haikuwa hivi miaka kumi iliyopita. Sababu kubwa iliosababisha ripoti hizi za CAG ziwe na mvuto wa aina yake kwa makundi hayo ya jamii yaliyokwisha kutajwa ni pamoja na mwitikio chanya wa Serikali na Bunge katika kusimamia utekelezaji wa mapendekezo ya CAG. Haya kwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni mafanikio yasiyopaswa kuachwa kunukuliwa.



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli (kulia) akipokearipoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG)Prof. Mussa Assad kwa mwaka 2014/15, Ikulu, Dar es Salaam, Machi 2016*

- ✓ Mafanikio mengine ya ndani ya nchi ni kutoa ushauri unaotekelezeka. Pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoa Ripoti za ukaguzi, pia hutoa ushauri wa kiutendaji kwa wakaguliwa ambao hawakufanya vizuri, Ofisi imekuwa ikitoa mchango zaidi wa kiutaalamu kwa kuwashirikisha Wakaguliwa hao katika Warsha mbalimbali za uwajibikaji; Kukaa katika meza za majadiliano na wakaguliwa na kujadiliana kuhusu utendaji kazi wao. Aidha, katika Mpango Mkakati wake (2016/17-2020/21) Ofisi hii imejielekeza katika kufanya mazungumzo zaidi na taasisi zote zitakazopata Hati yenye Shaka kwa madhumuni kuangalia namna ya kuisaidia taasisi husika. Kwa takwimu za wazi hali halisi ya utekelezaji wa mapendekezo ya ripoti za CAG kwa ukaguzi wa fedha wa miaka iliyopita hadi kufikia tarehe 30 Juni 2015 ni kama ifuatavyo:

| Na. | Ripoti | Jumla ya Mapendekezo yaliyotolewa | Mapendekezo yaliyotekelezwa | Mapendekezo ambayo utekelezaji wake unaendelea | Mapendekezo ambayo utekelezaji wake haujaanza | Asilimia ya mapendezo yasiyotekelezwa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Serikali za Mitaa | 16 | 0 | 6 | 10 | **63%** |
| 2 | Serikali Kuu | 46 | 8 | 37 | 1 | **2%** |
| 3 | Mashirika ya Umma | 37 | 27 | 10 | 0 | **0** |
| | **Jumla** | **99** | **35** | **53** | **11** | **65** |
| | **Asilimia** | **100%** | **35%** | **54%** | **11%** | |

Aidha, kwa upande wa Ukaguzi wa Ufanisihalisi ya utekelezaji wa mapendekezo ya ripoti za CAG kwa kaguzi za Ufanisi hadi kufikia tarehe 31 Machi 2016 ni kama ifuatavyo:

| Ripoti Husika | Jumla | Mapendekezo yaliyotekelezwa | Mapendekezo Yaliyopo Kwenye Utekelezaji | Mapendekezo yasiyotekelezwa | Asilimia ya Mapendekezo yasiyotekelezwa |
|---|---|---|---|---|---|
| Usimamizi, Tathmini, na Mgawanyo wa Bajeti kwa Ajili ya Huduma za Mama Wajawazito Nchini | 19 | 9 | 9 | 1 | **5%** |
| Usimamizi wa Utoaji wa Malipo ya Pensheni kwa Wastaafu Nchini | 28 | 14 | 10 | 4 | **14%** |

| Ripoti Husika | Jumla | Mapendekezo yaliyotekelezwa | Mapendekezo Yaliyopo Kwenye Utekelezaji | Mapendekezo yasiyotekelezwa | Asilimia ya Mapendekezo yasiyotekelezwa |
|---|---|---|---|---|---|
| Usimamizi wa Makusanyo ya Mapato ya Ushuru Katika Serikali za Mitaa | 6 | 1 | 4 | 1 | **17%** |
| Usimamizi wa Ukarabati wa Magari Yanayomilikiwa na Taasisi za Serikali | 20 | 2 | 12 | 6 | **30%** |
| Usimamizi wa Uvunaji wa Mazao ya Misitu Nchini | 13 | 0 | 11 | 2 | **15%** |
| Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Maji Mijini | 27 | 3 | 22 | 2 | **7%** |
| **Jumla** | **113** | **29** | **68** | **16** | |
| **Asilimia** | **100%** | **26%** | **234%** | **24%** | |

- ✓ Mafanikio ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika ngazi ya kimataifa ni pamoja na kutoa ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi zenye ubora unaotambulika kimataifa. Kati ya ripoti 15 za Ukaguzi wa Ufanisi zilizotolewa na CAG kwa miaka 5 mfululizo, ripoti 2 ziliweza kushindanishwa katika ngazi ya ripoti bora kimataifa na kuweza kushinda tuzo ya Ripoti Bora ya Ukaguzi barani Afrika kwa Taasisi za Ukaguzi kwa nchi wanachama wanaozunguza kugha ya kiingereza (AFROSAI-E) kwa mwaka 2011 na 2015.

- ✓ Mafanikio mengine ya ngazi ya kimataifa nikuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mjumbe na Mwenyekiti wa Bodi ya Ukaguzi ya Umoja wa Mataifa (UNBoA). Uenyekiti wa Bodi ni wa kupokezana na kwa sasa nafasi hiyo ni yetu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Prof. Mussa J. Assad ndiyo Mwenyekiti wa Bodi ya Ukaguzi wa Umoja wa Mataifa nafasi aliyoipokea kutoka kwa Waingereza mwaka mmoja uliopita. Prof. Assad anakuwa Mtanzania wa kwanza kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Ukaguzi ya Umoja wa Mataifa. Dhamana hii iliyopewa nchi yetu ni kubwa mno kwani kuchaguliwa huku ni heshima sio kwa Prof. Assad tu bali ni kwa nchi na Watanzania kwa ujumla.

- ✓ Ukaguzi ni nyenzo muhimu katika kufanikisha ufanisi wa taasisi/shirika kufikia malengo yake. Kwa kuzikagua shughuli za Umoja wa Mataifa, Ofisi hii imeweza kuyasaidia Mashirika ya Umoja wa Mataifa kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yakeambayo ni kudumisha haki za binadamu

duniani, kuwalinda wahanga wa vita na machafuko, kusimamia wakimbizi na wanaokimbia vurugu za ndani (IDP), kudhibiti mazingira na mabadiliko ya tabia nchi, kusimamia haki na kupinga vitendo kandamizi, usawa wa jinsia na haki za watoto, kuhakikisha jumuiya ya kimataifa inafikia malengo ya maendeleo endelevu (SDG), kuondosha umaskini na maradhi duniani, kuhakikisha haki za makazi, kudhibiti idadi ya watu na uzazi salama. Fursa ya kuwa Mkaguzi wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa ni adhimu kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hata kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Umoja wa Mataifa.

- ✓ Katika kipindi cha ushiriki wake wa miaka minne sasa katika Bodi hii, Tanzania imekagua na kuandaa ripoti za Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Idadi ya Watu Duniani la Umoja wa Mataifa (UNFPA), Shirika la Ujenzi na Misaada la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wakimbizi wa Palestina na Mashariki (UNRWA), Mfuko wa Akiba kwa Watumishi wa UNRWA Wakazi (UNRWA – SPF), Shirika la Umoja wa Mataifa la Usawa wa Jinsia na Uwezeshaji wa Wanawake (UN – Women), Shirika la Ukuzaji Mitaji la Umoja wa Mataifa (UNCDF), Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Mazingira (UNEP), Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Makazi (UN Habitat), Mahakama za Kimataifa za Makosa ya Jinai za mauaji ya kimbari ya Rwanda (ICTR) na Yugoslavia ya zamani (ICTY), pamoja na Mpango wa Kuzipunguza Mahakama hizo (MICT). Vilevile kwa kipindi chote hiki, Tanzania ilishirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China na baadaye Serikali ya India katika kukagua vikosi vya Amani vya Umoja wa Mataifa katika sehemu mbalimbali duniani.




*Prof. Mussa J. Assad Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG na Mwenyekiti wa Bodi ya Ukaguzi ya Umoja wa Mataifa (UNBoA) akizungumza mbele ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Mhe. Ban Ki Moon, alipokuwa kwenye shughuli za Ukaguzi wa Bodi, mjini New York, Marekani, Julai, 2016*

## 8.0 MASUALA YANAYOPENDEKEZWA KUENDELEA KUBORESHWA

### 8.1 Mapato ya Serikali na Misamaha ya Kodi

Katika mwaka wa fedha 2014/15, Ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali umeonesha mapato halisi yaliyokusanywa kutokana na kodi yalikuwa shilingi trilioni 10.8 sawa na asilimia 89 ikilinganishwa na makisio yaliyopitishwa na Bunge ya shilingi trilioni 12 ambayo ni pungufu ya shilingi trilioni 1.2 sawa na asilimia 11.

Misamaha ya kodi sio kitu kigeni. Duniani nchi zina sera tofauti tofauti za misamaha ya kodi. Taarifa ya makusanyo ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2015 ilionesha kiasi cha misamaha ya kodi iliyotolewa kuwa ni Shilingi trilioni 1.6 sawa na asimilia 2 ya pato la ndani la Taifa. Kiwango hicho bado ni cha juu ikilinganishwa na lengo la Serikali la kupunguza misamaha hiyo kufikia kiwango kisichozidi asilimia 1 ya pato la ndani la Taifa. Katika kupunguza athari ni muhimu kwa serikali kuja na mfumo rafiki wa ulipaji kodi ambao kila mtu atajisikia vizuri kulipa.

**Deni la Taifa**

Kwenye ripoti za CAG, limekuwepo pia suala la ukuaji wa Deni la Taifa. Kimsingi, wakati serikali inapokopa fedha kwa sababu yoyote ile, deni hilo huhesabiwa kwenye Deni la Taifa. Deni la Taifa mara nyingi linakua kama serikali inajiingiza kwenye miradi mikubwa ya maendeleo ambayo gharama zake ni kubwa na serikali inakuwa haina fedha za kutosha kugharamia miradi ya aina hiyo. Kwenye miradi ya aina hii ni lazima serikali italazimika kukopa ili miradi hiyo ifanikiwe. Mfano ni Miradi ya ujenzi wa barabara za kisasa, mradi wa bomba la gesi Mtwara mpaka Dar es Salaam. Serikali ikiingia kwenye miradi mikubwa ya namna hiyo, ni lazima deni la taifa litaongezeka.

Kufikia tarehe 30 Juni, 2015 Deni la Taifa lilikuwa Shilingi trilioni 33.54. Katika hili, deni la ndani lilikuwa Shilingi trilioni 7.99 na deni la nje ni trilioni 25.55. Hili ni ongezeko la trilioni 7.05 sawa na asilimia 27 ikilinganishwa na deni la Shilingi trilioni 26.49 lililoripotiwa Juni 30, 2014.

Uchambuzi CAG umeonyesha kuwa malipo ya kugharamia madeni ya kiasi cha Shilingi trilioni 4.60 mwaka huu ni sawa na asilimia 46 ya makusanyo ya ndani ya Serikali ya Shilingi trilioni 10.8. Gharama hizo zikijumuisha na gharama nyingine

kama vile mishahara ya wafanyakazi na likizo, Serikali hubaki na kiasi kidogo cha fedha za kugharamia miradi ya maendeleo na huduma nyingine za kijamii.

Mapendekezo ya CAG kuhusu Deni la Taifa ni kwanza, Serikali idumishe jitihada za ndani zilizoanza za kuhamasisha ukusanyaji wa mapato ili kujenga wigo mpana wa kulipa madeni. Pili, Serikali iweke mpango maalum wa kimkakati kuhusu fedha ikiwa ni pamoja na kupunguza gharama na kuongeza mikopo yenye masharti nafuu, pamoja na kuratibu vizuri shughuli za fedha za kigeni hapa nchini ili kutilia mkazo kwa kuhakikisha kwamba ukuaji wa Deni la Taifa unaenda sambamba na maendeleo ya nchi.

### 8.2 Mafuta

Tanzania imejaliwa utajiri mwingi wa maliasili. Miaka michache huko nyuma, Tanzania ilikuwa miongoni mwa wazalishaji wakuu wa madini ya dhahabu duniani na miaka michache ijayo tunaweza tukajikuta kwenye uchumi wa kati wa mafuta na viwanda kama Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anavyosisitiza.

Aidha, kwenye baadhi ya ripoti za CAG alizotoa miaka ya nyuma aliainisha maeneo ambayo yalionekana na mapungufu kama vile maeneo ambayo serikali ilipanga mrahaba lakini ilishindwa kuukusanya. Mara baada ya kubaini mapungufu yaliyokuwepo kwenye sera na sheria zilizotawala eneo la madini, wapo baadhi ya Watanzania ambao walikuwa wanadhani kuwa suluhu ni kuvunja mikataba ile inayoonekana kuwa na mapungufu. Kwa nchi inayofuata mfumo wa kisheria, ukishaingia mkataba ni lazima uufuate.

Ni mapendekezo yetu kwa Serikali kuwa Mikataba inayosainiwa ni muhimu kuwekwa wazi kwa vyombo mbalimbali vya udhibiti nchini ikiwemo Bunge, Taasisi Simamizi na hata Umma kwa ujumla. Vilevile, ni muhimu kwa pande zote mbili kuingia kwenye mikataba baada ya kujiridhisha na kilichomo.

## 9.0 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kuimarisha udhibiti wa mapato na matumizi ya serikali, hata hivyo bado zipo changamoto mbalimbali. Baadhi ya changamoto zinazoikabili Ofisi hii ni pamoja na:

- ✓ Jamii kutofahamu mipaka ya kiutendaji ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Ni matamanio ya wananchi wengi kuwa mara ukaguzi unapokamilika,Ofisi hii ipewe mamlaka zaidi ya kupeleka watu mahakamani. Utaratibu huu kwa

nchi zinazofuata mfumo wa utawala bora ni utaratibu hatari kwani iwapo taasisi moja itapewa nguvu isiyodhibitika huweza kutumia vibaya madara yake na hivyo kusababisha hasara kwa taifa.

- ✓ Rasilimali Fedha, Rasilimali Watu na vitendea kazi ni miongoni mwa changamoto ambazo zimeendelea kuikabili Ofisi hii. Bajeti inayotolewa ni ndogo ukilinganisha na mahitaji halisia ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii. Miaka ya hivi karibuni kumekuwepo ongezeko la Kaguzi Maalum ambazo zinahitaji rasilimali fedha, rasilimali watu pamojana vitendea kazi kama vile magari, kompyuta mpakato, kamera za ushahidi n.k. Ukaguzi bila uwepo wa rasilimali zote hizo hauwezi kuwa na matokeo halisi yenye kuleta tija kwa mkaguliwa na nchi. Hata hivyo, juhudi za kuendelea kuzungungumza na Serikali zinaendelea ili kuangalia namna ambavyo Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaendelea kuimarishwa.

## 10.0 HITIMISHO

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inatoa rai kwa wananchi wote kuendeleza na kukuza maadili na nidhamu ili kupunguza ongezeko la matukio ya ubadhirifu sanjari na kuzihusisha mamlaka za usimamizi na uchunguzi kikamilifu ikiwa ni pamoja na kutoa mrejesho au ushirikiano pale inapohitajika ili zitekeleze majukumu yake kwa ufasaha zaidi na si vinginevyo.

Kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, Ofisi imejiwekea dira ya kuwa kituo bora cha ukaguzi wa hesabu katika sekta ya umma. Ili kufanikisha lengo hilo ofisi itaendelea kutumia njia mbalimbali kama sehemu ya mikakati yake ikiwemo kuelimisha umma kuhusu majukumu ya ofisi; kujenga uwezo wa maarifa kwa watumishi; kusimamia misingi ya nidhamu na maadili pamoja kuimarisha ushirikiano na wadau wa ndani na nje ya ofisi kwa lengo la kukuza uelewa na kujenga misingi ya uwajibikaji na utawala bora.



**Prof. Mussa J. Assad**
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**